Imehuishwa mara ya mwisho tarehe: 31.01.2026
Masharti haya ya Jukwaa la Huduma yanawahusu watu binafsi ("Wateja") wanaojiandikisha kwenye Jukwaa la Bolt ili kupata na kupitia fursa zilizopo Tanzania za kuomba Huduma za Usafiri Mtandaoni.
Maneno na misemo yaliyoandikwa kwa herufi kubwa katika Masharti haya ya Jukwaa yana maana kama ilivyotolewa kwenye farahasa kwenye kipengele cha {15} hapa chini.

Unaweza kupakua toleo la nje ya mtandao la Masharti haya ya Jukwaa kwa ajili ya kumbukumbu na matumizi yako ya baadae hapa.

**1. Kuhusu Bolt na uhusiano na wewe**

Muhtasari

1.1. Bolt inaendesha jukwaa la mtandaoni ndani ya Tanzania ('Jukwaa la Bolt') linalounganisha na kulinganisha watoa huduma za usafiri wanaojitegemea ('Watoa Huduma') na wateja watarajiwa ('Wateja').

1.2. Kama Mteja unaweza kufikia Jukwaa la Bolt kwa mujibu wa Masharti haya ya Jukwaa ili kupitia, na ukiamua, kuomba na kununua Huduma za Usafiri Mtandaoni kutoka kwa Watoa Huduma. Ada za ziada, kama vile ada za kughairi au ada za usafi, zinaweza pia kutozwa kama ilivyobainishwa katika kipengele cha {5}.

1.3. Makubaliano yoyote yanayohusu utoaji wa Huduma za Usafiri Mtandaoni yatafanyika kati yako na Mtoa Huduma husika. Pale tunapokusanya malipo kutoka kwako kwa niaba ya Watoa Huduma, tutafanya hivyo kama wakala wao aliyeteuliwa.

1.4. Aidha, Bolt inaweza kukutoza Ada za Jukwaa kwa huduma tutakazokupatia kama ilivyoainishwa katika kipengele cha {6}.

1.5. Tutachakata taarifa zako binafsi kwa mujibu wa ilani ya faragha ya Tanzania inayopatikana katika tovuti https://bolt.eu/privacy.

1.6. Ni lazima uwe na umri wa angalau miaka 18 ili kujiandikisha kama Mteja na kutumia Programu ya Mteja.

Majukumu ya Bolt kama wakala wa Watoa Huduma

1.7. Kwa kufikia Jukwaa la Bolt, Watoa Huduma wametuteua kama wakala wao kwa ajili ya kujadiliana mikataba ya Huduma za Usafiri Mtandaoni inayofanyika kati ya Watoa Huduma na Wateja. Idhini hii inaturuhusu kufanya majukumu kama vile:

1.7.1. kukulinganisha wewe na Madereva, kama ilivyoelezwa katika kipengele cha {5};

1.7.2. kupiga hesabu na kutoa taarifa kuhusu Nauli, pamoja na makadirio ya Nauli na Malipo ya Tozo husika, zinazopaswa kulipwa katika Huduma za Usafiri Mtandaoni;

1.7.3. kupanga ukusanyaji wa Nauli, Ada za Kughairi/Ada za Fidia na Ada za Usafi unazopaswa kulipa kwa Watoa Huduma, na kupeleka malipo hayo kwa Watoa Huduma; na

1.7.4. kutoa stakabadhi na ankara kwa niaba ya Mtoa Huduma.

1.8. Tafadhali fahamu kwamba Watoa Huduma:

1.8.1. lazima walipe kamisheni kwa Bolt kwenye malipo yanayofanywa na Wateja kutokoana na Huduma za Usafiri Mtandaoni;

1.8.2. hawalazimiki kufikia Jukwaa la Bolt ili kutoa Huduma za Usafiri Mtandaoni; na

1.8.3. hawazuiwi kutoa huduma za usafiri mtandaoni nje ya Jukwaa la Bolt.

**2. Kuhusu Masharti haya ya Jukwaa na Jukwaa la Bolt**

2.1. Masharti haya ya Jukwaa:

2.1.1. yataanza kutumika na kukubana kuanzia tarehe 31.01.2026 au kuanzia tarehe uliyojiandikisha kwa mara ya kwanza kama Mteja — yoyote ya baadae;

2.1.2. yataendelea kutumika mpaka yatakapositishwa na wewe au Bolt kulingana na kipengele cha {11}; na
2.1.3. yatachukua nafasi ya matoleo yaliyopita ya Masharti ya Jukwaa, vovyote vile ilivyoelezwa.
2.2. Bolt inaweza kufanya mabadiliko kwenye Masharti haya ya Jukwaa na/au Jukwaa la Bolt kwa kukupatia notisi ya muda unaofaa kabla ya mabadiliko hayo kuanza kutumika. Kama huafiki makubaliano hayo, unaweza kusitisha uhusiano wako na Bolt kulingana na kipengele cha {11}.
2.3. Bolt pia inaweza kufanya mabadiliko kwenye Masharti haya ya Jukwaa au matumizi yako ya Jukwaa la Bolt mara moja na bila kukupa notisi ya awali pale:
2.3.1. unakubaliana na mabadiliko;
2.3.2. tunapofanya mabadiliko, maboresho au marejeo ya Jukwaa la Bolt ambayo ni ka ajili ya urembo pekee, kuboresha utendaji au kwa ulinganisho hayana madhara makubwa kwa matumizi yako ya Jukwaa la Bolt;
2.3.3. tunapofanya mabadiliko tofauti na yaliyotajwa kwenye kipengele cha {2.3.2}, kuanzisha muonekano wa muda mfupi kwa ajili ya kupima, kujaribu, upatikanaji wa awali, kuhakiki au maendeleo;
2.3.4. mabadiliko yanatakiwa haraka ili kukidhi matakwa ya sheria au kanuni husika; au
2.3.5. tunachukua hatua za tahadhari kukabiliana na hatari kwa Watumiaji, hatari za usalama wa mtandaoni (ikiwemo programu hasidi, barua taka au ukiukwaji wa data) au sughuli inayoshukiwa kuwa haramu au kinyume cha sheria.
2.4. Bolt inapofanya mabadiliko kwa mujibu wa vipengele vya {2.3.3} mpaka {2.3.5} (kwa pamoja), itakutaarifu kuhusu mabadiliko husika haraka iwezekanavyo.
2.5. Maudhui na utendaji wa Jukwaa la Bolt vinatolewa katika msingi wa “kama ilivyo” na “kama invyopatikana”. Kwa kufikia na kuruhusu wengine kufikia Jukwaa la Bolt, unatambua kuwa:
2.5.1. Bolt haikuhakikishii, waziwazi au kwa kudokeza, juu ya upatikanaji wa Jukwaa la Bolt, maudhui yake au utendaji wake; na
2.5.2. Bolt inaweza mara kwa mara kubadili muonekano uliopo kwa muda mfupi katika hatua ya upimaji, kujaribu, ufikiaji wa awali, uhakiki au maendeleo.

**3. Haki zako kufikia Jukwaa la Bolt**
3.1. Chini ya Masharti haya ya Jukwaa, tunakupa haki ya kutumia Jukwaa la Bolt isiyo ya kipekee, bila kizuizi, inayoweza kubatilishwa, na bila mrabaha, kwa madhumuni ya:
3.1.1. kufikia na kupitia fursa ili kutoa Huduma za Usafiri Mtandaoni; na
3.1.2. kuomba Huduma za Usafiri Mtandaoni kwa hiyari yako.
3.2. Haki yako ya kufikia Jukwaa la Bolt kupitia na kuomba Huduma za Usafiri Mtandaoni inatolewa tu:
3.2.1. kwa wakati ule unapoweza kuthibitisha utambulisho wako na/au taarifa za kuingia kwenye mfumo, ili kuzuia ufikiaji usioidhinishwa;
3.2.2. kuhusiana na ufikiaji wa Kundi lolote, ili mradi umekidhi vigezo husika vinavyotakiwa kwenye Kundi, kama vipo;
3.2.3. kwa wakati ule tu matumizi ya Jukwaa la Bolt hayatasababisha madhara makubwa kwa uadilifu au sifa yake.
3.3. Kwa madhumuni ya pekee ya kuzuia ufikiaji usioidhinishwa, Bolt inaweza mara kwa mara kuwataka Watumiaji kuthibitisha utambulisho wao na/au taarifa za kuingia kwenye mfumo.

**4. Taarifa zinazowasilishwa kwenye Jukwaa la Bolt**
4.1. Unapaswa kuhakikisha kwamba taarifa zote unawasilisha, au unazopanga kuziwasilisha,

kwa Bolt kuhusiana na matumizi ya Jukwaa la Bolt, kuwa sahihi muda wote. Hii inajumuisha, pale inapohitajika, jina lako, taarifa zako za mawasiliano, utambuzi wa picha, anwani, taarifa za kampuni, Njia ya Malipo na hali ya usajili wa kikodi. Unawajibika pia kuboresha au kuondoa taarifa zozote ambazo sio sahihi au hazihitajiki tena.

4.2. Unawajibika wewe mwenyewe kuhakikisha kuwa taarifa zote na maudhui uliyowasilisha au ulizopandisha kwenye Jukwaa la Bolt ni halali. Bolt inabaki na haki ya kuondoa maudhui yasiyo halali kutoka kwenye Jukwaa la Bolt muda wowote. Endapo hii ikitokea, utakuwa na haki ya kupinga kulingana na kipengele cha {14.8}.

4.3. Tafadhali tambua kuwa Bolt inaweza, baada ya kutoa onyo la awali, ikasitisha kufanyia kazi pingamizi ikiwa itaonekana kuwa malalamiko yasiyo ya msingi yatakuwa yameletwa mara kwa mara, kwa kuangalia uwingi wake, kiwango, ubaya, na kwa nia mbaya.

**5. Huduma za Usafiri Mtandaoni**

Muhtasari

5.1. Kwa mujibu wa Masharti haya ya Jukwaa, unaweza kufikia Jukwaa la Bolt na kuomba Huduma za Usafiri Mtandaoni na baada ya hapo kuweza kuingia makubaliano na Watoa Huduma kwa ajili ya kupata huduma hizo.

5.2. Unaweza kuomba Huduma za Usafiri Mtandaoni kutolewa mapema, au pale zinapopatikana, kwa muda maalum.

5.3. Wateja wanapswa kuthibitisha mapema kupitia Jukwaa la Bolt kama watalipia Huduma za Usafiri Mtandaoni:

5.3.1. kupitia kwenye Jukwaa la Bolt (ambapo Bolt itapanga kukusanya malipo stahiki kwa Watoa Huduma kama wakala, kwa mujibu wa kipengele cha {7})

5.3.2. kwa pesa taslimu (kwa kumlipa Dereva husika, anayekusanya malipo kwa niaba ya Mtoa Huduma).

5.4. Tafadhali fahamu kwamba Watoa Huduma na Madereva ni wahusika wa tatu ambao hawako chini ya udhibiti wa moja kwa moja wa Bolt. Wanaweza kufuta, kukataa au kutoingia kwenye makubaliano ya Huduma za Usafiri Mtandaoni pale inapokuwa halali kufanya hivyo.

Maombi ya Huduma za Usafiri Mtandaoni

5.5. Katika kujibu maombi ya Huduma za Usafiri Mtandaoni yaliyofanywa na Wateja, Bolt ikifanya kazi kama wakala aliyeteuliwa wa Watoa Huduma:

5.5.1. itaamua makadirio ya Nauli kwa ajili ya Huduma za Usafiri Mtandaoni yatakayokubaliwa kati ya Wateja na Watoa Huduma, kwa kuzingatia:

5.5.1.1. njia na muda wa Huduma ya Usafiri Mtandaoni iliyoombwa route;

5.5.1.2. (pale inapohusika) Kundi la huduma iliyoombwa na Mteja;

5.5.1.3. (pale inapohusika) endapo Mteja ameomba kuchukuliwa haraka au ameomba kuchukuliwa kwa muda uliopangwa; na

5.5.1.4. sababu nyingine za kisoko kama vile upatikanaji na uhitaji wa Madereva.

5.5.2. kulingana na vipengele vya {5.6}, {5.7} and {5.8}, kuwakaribisha Madereva waliopo karibu sana na eneo la kuchukulia kuonyesha utayari wao kutoa Huduma ya Usafiri Mtandaoni, kwa kuzingatia (kwa madhumuni ya kuamua mpangilio na/au muda wa maombi hayo):

5.5.2.1. sababau zilizoainishwa katika kipengele cha {5.5.1};

5.5.2.2. (pale inapokuwepo) ombi lolote la Mteja la kupata gari maalum; na

5.5.2.3. sababu nyingine zinazolenga kuharakisha mpangilio unaowezekana wa Huduma za Usafiri wa Mtandaoni, ikiwemo kadirio la muda wa Madereva kufika kwenye eneo la kuchukulia na pia endapo Madereva wanatoa Huduma za Usafiri Mtandaoni kwa muda huo.

5.6. Katika baadhi ya maeneo yenye uhitaji mkubwa na idadi kubwa wa Watumiaji, kama viwanja vya ndege, Bolt inaweza kutekeleza mfumo wa foleni wa “wa kwanza kuingia, wa

kwanza kutoka" katika kuwaalika Madereva kuonesha utayari wao kutoa Huduma za Usafiri Mtandaoni.

5.7. Ili kuharakisha upangaji wa Huduma za Usafiri Mtandaoni na kupunguza chaguzi zisizofaa, Bolt inaweza kuzingatia mazingira ambapo kuna mahusiano hasi, mrejesho au malalamiko yaliyowahi kutokea baina ya Mteja husika na Dereva husika.

5.8. Pale inapowezekana, Madereva wanaweza kurekebisha makaribisho wanayoyapokea kwa kuweka vichujio na vigezo ikiwemo vipengele vya bei vinavyopendekezwa au umbali kutoka maeneo ya kuchukuliwa.

5.9. Pale inapohusika, ni lazima umlipe Dereva Ada ya Kughairisha/Ada ya Fidia pale unapoghairi safari kwa mujibu wa vipengele vya {5.15} na {5.16}.

5.10. Unakubali kuwa makubaliano yoyote ya Huduma za Usafiri Mtandaoni yaliyofikiwa kati yako na Watoa Huduma yatatekelezwa kwenye sehemu ya kuchukulia Abiria au mizigo (yaani baada ya kuanza kuanza Kipindi cha Safari husika).

5.11. Endapo Huduma za Usafiri Mtandaoni itaanza kutolewa, utakubali kumlipa Mtoa Huduma:

5.11.1. Nauli, kama kama inavyoonyeshwa katika Programu ya Mteja kabla ya kuanza kutolewa kwa Huduma ya Usafiri Mtandaoni; na

5.11.2. (kama inahusika) Ada ya Usafi, kwa mujibu wa kipengele cha {5.16}.

5.12. Tafadhali fahamu kuwa Watoa Huduma na Madereva wanaotenda kwa niaba yao wanaweza kughairi, kukataa au kukataa kuingia makubaliano ya Huduma za Usafiri Mtandaoni wakati wowote, isipokuwa pale wanapolazimika kutoa huduma kwa mujibu wa sheria au kanuni zilizotolewa na mamlaka za udhibiti.

5.13. Pale Huduma za Usafiri Mtandaoni zimekamilika (au zimeisha kwa namna yoyote), Nauli husika itakokotolewa kwa misingi iliyoonyeshwa kwenye Pogramu ya Mteja kabla ya kuanza kwa Huduma ya Usafiri Mtandaoni.

5.14. Bolt haizuii au kuingilia na masharti ya ziada ya huduma yaliyokubaliwa kati ya Wateja na Watoa Huduma kwa ajili ya Huduma za Usafiri Mtandaoni, isispokuwa pale kufanya hivyo kutakinzana na Masharti haya ya Jukwaa au masharti ya jukwaa yanayotumika kwa Watoa Huduma. Endapo kuna masharti ya ziada yamekubaliwa kati yako na Mtoa Huduma, tunapendekeza uhifadhi kumbukumbu za makubaliano hayo kwa ajili ya matumizi ya baadae. Bolt haitaingilia endapo kutakuwa na mgogoro unaohusika na makubaliano ya namna hiyo.

Ada za Kughairisha/ Ada za Fidia

5.15. Ada za Kughairisha/Ada za Fidia unazotakiwa kulipa kwa Mtoa Huduma, kama umeghairi maombi (au kwa namna yoyote umeshindwa kuingia makubaliano) ya Huduma za Usafiri Mtandaoni baada ya kuisha kwa Kipindi cha Kutafakari, itaonyeshwa kwenye Programu ya Mteja na inaweza kutofautiana kulingana na aina ya Kundi na/au huduma husika.

5.16. Jukumu la Bolt kukusanya Ada ya Kughairi/Ada ya Kufidia linatokea pale tu Mtoa Huduma kwa nia njema altaka kutoa Huduma husika ya Usafiri Mtandaoni. Kama unaamini kuwa umetozwa Ada ya Kughairi/Ada ya Fidia kimakosa, tafadhali wasiliana na timu yetu ya usaidizi.

Ada za Usafi

5.17. Unakubali kuwa Mtoa Huduma anaweza kukutoza Ada ya Usafi pale ambapo gari litaachwa na uchafu, madoa au kuchafuliwa kama matokeo ya Huduma za Usafiri Mtandaoni ulizoomba. Utatakiwa kulipa Ada ya Usafi mara tu inapotakiwa. Kwa dhumuni hili, Watoa Huduma wanaiteua Bolt kukusanya mpaka kiasi cha shilingi za Kitanzania elfu kumi (TZS 10,000) kwa niaba yao, na unakubali kuwa tunaweza kukusanya Malipo kwa kiasi hiki pale inapohitajika kwa mujibu wa kipengele cha {7}. Kwa ufafanuzi, hii haimzuii Mtoa Huduma au mtoa bima wao kudai madai ya ziada moja kwa moja kutoka kwako, kwa mfano pale uharibifu ni mkuwa, na ni halali kufanya hivyo.

Kufanya malipo kwa Watoa Huduma

5.18. Pale unapofanya malipo kwa Watia Huduma kupitia Jukwaa la Bolt, Bolt itakusanya malipo unayotakiwa kuwalipa Watoa Huduma kuhusiana na Huduma za Usafiri Mtandaoni kwa fedha taslimu kulingana na kipengele cha {7}. Pale unapokubali kulipia Huduma za Usafiri Mtandaoni kwa fedha taslimu, ni jukumu lako mwenyewe kuhakikisha kuwa unatoa kiasi husika cha fedha taslimu kwa Dereva (Madereva).

5.19. Kwa kuomba Huduma za Usafiri Mtandaoni, unakubaliana na Bolt kwamba utazingatia majukumu yako ya kufanya malipo kwa Watoa Huduma pale inapohitajika. Endapo utashindwa kufanya malipo unayodaiwa na Watoa Huduma, unaweza ukapoteza kufikia Jukwaa la Bolt au unaweza kuzuiwa kufanya malipo kwa njia maalum (mfano kufanya malipo kwa fedha taslimu).

Ufikiaji wa Makundi

5.20. Bolt inaweza kutengeneza makundi tofauti ya huduma katika soko ili kuoanisha: (i) Watoa Huduma kuwa na uwezo wa kukamilisha huduma kwa kulingana na Kundi husika, na (ii) Wateja wanaochagua huduma inayotolewa kulingana na Kundi husika (ii) Wateja wanaochagua huduma inayotolewa kulingana na Kundi husika. Kwa mfano, kama ‘gari inayotumia umeme’ ipo, Bolt inaweza kulenga kuwaunganisha Wateja kwa Watoa Huduma wenye wanaotumia gari inayotumia umeme. Makundi ya huduma yanaweza pia kuonyesha aina ya huduma, kama vile Huduma za Usafirishaji (tazama kipengele cha {5.25} mpaka {5.29}).

5.21. Makundi yaliyopo kwa Dereva yatategemea mambo husika kulingana na kila aina na uhitaji wake sokoni (kwa mfano, Dereva ni lazima kutumia gari la umeme ili aweze kufikia Kundi la gari linalotumia umeme).

5.22. Kwa taarifa zaidi kuhusiana na Makundi yaliyopo kwenye soko husika, tafadhali wasiliana na timu yetu ya usaidizi.

Ofa

5.23. Bolt inaweza, kwa hiari yake, kutoa Ofa zilizopo kwa Wateja ambapo Bolt itatoa faida kwa matumizi yao ya Jukwaa la Bolt.

5.24. Pale Ofa inapotolewa kwa Wateja:

5.24.1. Kupokea faida kutategemea kukamilika kwa mahitaji husika kwenye ofa husika.

5.24.2. Ofa itaendana na kukidhi Masharti haya ya Jukwaa. Bolt inabaki na haki ya kuzuia faida ya ofa pale ambapo kutakuwa na uvunjwaji wa Masharti haya ya Jukwaa , ikiwemo pale ambapo wewe au Abiria yeyote amejihusisha na Kitendo cha Udanganyifu kilichopigwa marufuku.

5.24.3. Kufikia Jukwaa haitakuwa na sharti la wewe kushiriki au kukamilisha ofa yoyote.

Huduma za Usafirishaji

5.25. Pale Bolt inawezesha Kundi la Huduma za Usafirishaji liwepo kwa Watumiaji, Mteja anaweza kuomba usafirishaji wa bidhaa kutoka eneo la kupokelea hadi sehemu ya hitimisho bila usafirishaji wa Abiria.

5.26. Huwezi kuomba au kutumia Huduma za Usafirishaji kwa madhumuni ya kusafirisha bidhaa zifuatazo:

5.26.1. vitu vyenye uzito wa zaidi ya kilo kumi na tano (15);

5.26.2. pesa taslimu (pamoja na pesa zozote za kigeni), kadi za malipo, dhamana, au vocha za zawadi;

5.26.3. silaha za moto na vifaa vingine vilivyotengenezwa mahususi kwa ajili ya kushambulia au kujilinda;

5.26.4. vifaa vinavyoweza kuwaka, mionzi, sumu, au vifaa vya hatari vinavyofanana na hivyo;

5.26.5. chakula na vinywaji (ikiwa ni pamoja na vilevi/pombe);

5.26.6. Wanyama, binadamu na viumbe vingine vilivyo hai au visivyo hai, pamoja na sehemu zake, mabaki, vimiminika au vitu vinavyotokana na wanyama, binadamu au viumbe vingine.

5.26.7. madawa ya kulevya, dawa, au vifaa vya matibabu;
5.26.8. bidhaa zenye thamani zaidi ya Shilingi za Kitanzania Laki Tatu;
5.26.9. vifaa ambavyo haviwezi kusafirishwa bila ya kuwa na leseni za nyongeza au vibali;
5.26.10. vifaa vikubwa au dhaifu ambavyo havifai kusafirishwa kwenye gari; na
5.26.11. bidhaa haramu, zilizoibiwa au zisizoruhusiwa kisheria.
5.27. Watoa Huduma na Wateja wanahimizwa kukataa na kusitisha Huduma zozote za Usafirishaji zinazohusu bidhaa zozote zilizotajwa katika kipengele cha {5.26}. Endapo utajaribu kusafirisha bidhaa hizo, unaweza kupoteza Kufikia Jukwaa la Bolt.
5.28. Pale unapoomba au kununua Huduma za Usafirishaji unakubali kuwa ni jukumu lako pekee kuhakikisha kuwa bidhaa zitakazosafirishwa:
5.28.1. zimefungwa vizuri ili kuepusha uharibifu wakati wa safari;
5.28.2. zimeandaliwa na kuwekwa kwa ajili ya kusafirishwa kwa usalama na kuchukuliwa kwa haraka na Dereva anapofika;
5.28.3. zinakabidhiwa moja kwa moja kwa Dereva husika pekee; na
5.28.4. zinaweza kuchukuliwa kwa usalama, au kuhifadhiwa baada ya kuwasilishwa na Dereva husika kwenye eneo la kuchukuliwa.
5.29. Kwa taarifa zaidi kuhusiana na Huduma za Usafirishaji, tafadhali wasiliana na timu yetu ya usaidizi.

**6. Ada za Jukwaa**

6.1. Zaidi ya kiasi kinachotozwa na Watoa Huduma kwa Huduma ya Usafiri Mtandaoni, unawezwa kutozwa Ada za Jukwaa na Bolt. Ada hizi zinachangia uendeshaji, matengenezo, na uboreshaji wa jukwaa. Ada hizi zinaweza kujumuisha ad ana tozo za serikali, kodi au ada zingine zinazoendana na hizi. Kiasi cha Ada za Jukwaa kinaweza kubadilika mara kwa mara.
6.2. Endapo Ada ya Jukwaa inahusika na inatakiwa kulipwa na wewe:
6.2.1. itaonyeshwa kwenye makadirio la jumla ya gharama uliyooonyeshwa kabla ya kuomba Huduma za Usafiri Mtandaoni; na
6.2.2. italipwa kwa Bolt pale Huduma husika za Usafiri Mtandaoni zimeanza.
6.3. Kwa ajili ya kuondoa shaka, Ada za Jukwaa hazitozwi kwa ajili ya Huduma za Usafiri Mtandaoni au hwa ajili ya haki yoyote ya kutumia haki za mali miliki.

**7. Malipo**

7.1. Ili kuomba huduma kupitia Jukwaa la Bolt, Bolt inaweza ikakutaka kusajili angalau Njia ya Malipo moja iliyo halali. Unatuidhinisha kuhifadhi taarifa za Njia ya Malipo ulizotoa kwa ajili ya matumizi yako ya Jukwaa la Bolt.
7.2. Bolt inaweza ikachukua hatua moja au zaidi za uhakiki ili kuthibitisha uhalali wa Njia ya/za Malipo. Hii inaweza kujumuisha kuidhinisha Njia yako ya Malipo kwa muamala mmoja au miwili kwa kiasi kidogo, ambayo tutakuomba uthibitishe. Kiasi chochote kitakachoshikiliwa kwa madhumuni hayo kitaachiwa.
7.3. Kwa malipo yatakayofanyika kupitia Jukwaa la Bolt, unaiidhinisha Bolt mara moja:
7.3.1. Kukusanya Malipo yote kutoka kwenye Njia ya Malipo uliyochagua mara tu pale yanapotakiwa kulipwa; na
7.3.2. utaanda idhini ya awali kwa Malipo yanayotarajiwa kabla ya kukamilika kwa huduma yoyote, pale inapohusika, kutoka kwenye Njia ya Malipo uliyochagua.
7.4. Endapo Bolt haitafanikiwa kukusanya Malipo yotote kutoka kwenye Njia ya Malipo uliyochagua:
7.4.1. unatuidhinisha kukusanya Malipo ambayo hayajalipwa wakati utakapoomba huduma nyingine baadaye kupitia Jukwaa la Bolt; na

7.4.2. tunaweza kusimamisha kwa muda ufikiaji wako wote au kwa sehemu kwenye Jukwaa la Bolt mpaka pale Malipo kamili yatakapofanyika.
7.5. Bolt inaweza kuchukua hatua zinazofaa kurekebisha makosa yoyote kwenye malipo at kwenye kutoza ikijumuisha kufanya miamala ya kuongeza au kupunuza salio kwenye Njia ya Malipo. Endapo utapokea kiasi chochote kutoka kwetu kimakosa, unakubali kututaarifu mara moja na kurudisha mara moja kiasi hicho baada ya sisi kutoa maombi kupitia taarifa za malipo tutakazokupatia.
7.6. Unapokubali kufanya malipo ya Huduma za Usafiri Mtandaoni kwa fedha taslimu, ni jukumu lako mwenyewe kuhakikisha kuwa unatoa kiasi husika kwa fedha taslimu kwa Dereva/Madereva.
7.7. Pale inapohusika, Bolt itatoa risiti na/au ankara kwa niaba ya Watoa Huduma kwa njia ya mfumo wa kieletroniki.
7.8. Bolt inaweza kufuta, kusitisha, kuweka kikomo au kukataa malipo uliyofanya endapo Bolt ina sabau za msingi kuhisi kuwa malipo hayo au makusanyo yatakuwa yamefanywa kwa makosa au kinyume cha sheria, yanahusiana na Vitendo vya Udanganyifu Vilivyokatazwa au siyo halali au yamekatazwa kwa vikwazo vya kimataifa.
7.9. Pale inapowezekana, Bolt itawasiliana na wewe mapema kukutaarifu kutokea kwa masuala yoyote yaliyotajwa katika kipengele cha {7.9} na, pale inapohuskia, itajaribu kutatua masuala hayo, isipokuwa kama imekatazwa na matakwa ya mamlaka za udhibiti na kisheria, au pale Bolt imeshauriwa na chombo chenye mamlaka, mtoa huduma za malipo, au mshauri wa kisheria kutokufanya hivyo.
7.10. Una jukumu la kuchagua Njia ya Malipo uliyopendelea na iliyo sahihi pale unapofanya Malipo kupitia Jukwaa la Bolt. Bolt haitakubali maombi ya kubadilisha Njia ya Malipo baada ya ombi kufanyika, kwa sababu haijateuliwa na Watoa Huduma kufanya hivyo.
7.11. Tafadhali tambua kwamba endapo tutakusanya Malipo kutoka kwako kwa niaba ya Watoa Huduma, majukumu yako kwa Watoa Huduma husika yanakuwa yametimizwa pale ambapo Malipo yamewekwa kwenye akaunti zetu.

**8. Marufuku ya jumla**
8.1. Usitumie, au kuruhusu matumizi ya, Jukwaa la Bolt kujihusisha na, au kwa sababu yoyote inayohusiana na:
8.1.1. kitendo chochote kinyume cha sheria au haramu - ikiwemo kushirikiana maudhui, taarifa, au bidhaa zilizozuiliwa kwenye sheria zilizopo, au kuchakata taarifa binafsi kusiko halali; au
8.1.2. Vitendo vya Udanganyifu Vilivyopigwa Marufuku.
8.2. Wakati wa Vipindi vyote vya Maombi ya Huduma, hutakiwi - na unapaswa kuhakikisha Abiria anayehusiana na wewe – hausababishi hatari za kiusalama zisizo la lazima kwa Watumiaji, ikiwa ni pamoja na:
8.2.1. Kusababisha hatari za kusalama kwa Watumiaji wengine, ikiwemo
8.2.1.1. kumsumbua Dereva bila sabau yoyote ya msingi;
8.2.1.2. kumshawishi mtu yeyote kuendesha kinyume cha sheria za usalama barabarani au taratibu za usalama zilizotolewa na mamlaka za usimamizi;
8.2.1.3. kuwaweka wazi Watumiaji kwa silaha au vifaa vingine hatarishi bila ulazima; au
8.2.1.4. kutenda kwa namna nyingine katika hali ya kizembe ambayo haizingatii usalama wa Watumiaji wengine;
8.2.2. kujihusisha au kushawishi:
8.2.2.1. tabia ya hatari, ugomvi au inayotisha;
8.2.2.2. tabia yoyote ya Kibaguzi;
8.2.3. kusababisha wasiwasi mkubwa na usio wa lazima wa usalama au kukosa amani kwa

Watumiaji wengine, ikiwemo:
8.2.3.1. mawasiliano yasiyohitajika au ushawishi wa ngono unaofanya wengine kukosa amani, usalama au kujisikia vibaya; au
8.2.3.2. kuwaweka watu wengine katika hali zisizofaa au zisizokubalika, kama vile harufu mbaya.
8.3. Utendaji sahihi wa Jukwaa la Bolt unategemea Watumiaji wote kutumia kwa 'nia njema' na kuwa na kuwajali wengine. Kwa sababu hiyo, hupaswi kutumia Jukwaa la Bolt, au kuruhusu matumizi yake, katika njia yoyote ambayo mara kwa mara inavuruga, inaingilia, au kuchelewesha Huduma za Usafiri Mtandaoni kwa Watumiaji, au mlinganisho wa utayari kwa Wateja na Watoa Huduma kwa Bolt (kama ilivyoelezwa katika kipengele cha {5}), ikiwa ni pamoja na:
8.3.1. kughairi Huduma za Usafiri Mtandaoni kulikozidi baada ya kuziomba;
8.3.2. kubaki mtandaoni kwenye Programu ya Mteja kulikozidi wakati wa vipindi visivyo na shughuli;
8.3.3. kuchelewa mara kwa mara kughairi Huduma za Usafiri Mtandaoni baada ya kuamua kuwa hazihitajiki;
8.3.4. kuomba Madereva kughairi Huduma za Usafiri Mtandaoni, badala ya kughairi ipasavyo kupitia Programu ya Mteja, baada ya kuamua kutokuzikamilisha; au
8.3.5. kujihusisha kwa namna yoyote na Programu ya Mteja katika hali ambayo haiendani na uimara, lengo la nia njema kupitia, na pale inapohusika kutimiza, Maombi ya Huduma za Usafiri Mtandaoni.
8.4. Unapaswa usitoe, au kuruhusu utoaji wa, taarifa yoyote kupitia Jukwaa la Bolt zinazochanganya, za uongo, kinyume cha sheria au haramu.
8.5. Haupaswi kuruhusu mtu yeyote kufikia Jukwaa la Bolt kwa kutumia taarifa ambazo haziendani na taarifa zilizotolewa kwa Bolt kwa mujibu wa kipengele cha {4.1} ('taarifa binafsi'), ikiwemo kupitia namba yako/zako za simu au akaunti ya/za mitandao ya kijamii.
8.6. Haupaswi kujihusisha na, au kuruhusu, kujaribu:
8.6.1. kudanganya, kutumia isivyo sahihi, kuharibu, kukusanya taarifa yoyote iliyopo kwenye Jukwaa la Bolt;
8.6.2. kuharibu, kudanganya, au kuinglia mifumo ya usalama ya Jukwaa la Bolt;
8.6.3. kubadilisha, kuvunja, kutawanya, kugeuza ufundi au kujaribu kwa namna yoyote kupata namba ya chanzo ya sehemu yoyote ya Jukwaa la Bolt;
8.6.4. kufikia Jukwaa la Bolt kupitia njia yoyote tofauti na zile zilizotolewa na kuruhusiwa kupitia mifumo rasmi ya Bolt, tovuti au kwa njia nyingine yeyote; au
8.6.5. kujihusisha na matumizi mengine ya Jukwaa la Bolt ambayo yanaweza kuwa na madhara makubwa hasi katika ubora au hadhi ya Mfumo.
8.7. Ni jukumu lako kuhakikisha kuwa Abiria wanaosafirishwa kupitia ombi/maombi yako ya Huduma za Usafiri Mtandaoni hayakuweki katika mazingira ya wewe kuvunja Masharti haya ya Jukwaa.
8.8. Kwa kuondoa utatanishi, katazo la Tabia za Kibaguzi yaliyowekwa kwenye kipengele cha {8.2.2} halizuii haki yako ya kughairi maombi au kukuondoa katika muingiliano halali au kwa sababu za kisheria.
8.9. Bolt haina sera ya uvumilivu kwa tabia ya ugomvi, vitisho au udanganyifu. Haupaswi kuwatisha, kuwaogopesha, kuwalaghai kijanja au kuwaudhi wafanyakazi wowote, washirika au mawakala wa Bolt.

**9. Uchunguzi kuhusu tabia isiyo ya kawaida**

9.1. Endapo Bolt itapata taarifa inayoonesha uvunjifu wa wazi wa Masharti haya ya Jukwaa,

unapaswa kujiandaa kutoa ushirikiano wa kutosha katika uchunguzi wa msingi wa Bolt bila kuchelewa.
9.2. Unakubali kuwa Bolt inaweza kuomba mrejesho kutoka kwa Watumiaji ili kusaidia kutambua ukiukwaji wa Masharti ya Jukwaa.
9.3. Bolt inayo haki ya kutoa taarifa juu ya vitendo vyovyote visivyo halali, ambavyo sio vya kawaida au vyenye kutia mashaka kwenye vyombo husika vya dola au mamlaka za usimamizi bila kukupatia taarifa au kutoa taarifa kwa mtu mwingine.
9.4. Bolt inaweza kuhitajika kutoa taarifa za siri kwa mujibu wa na sheria husika, amri ya mahakama au vyombo vya uchunguzi.

**10. Jinsig ani upatikanaji wa Jukwaa la Bolt unavyoweza kusitishwa kwa muda**
10.1. Bolt ina mamlaka, kwa utekelezaji wa mara moja, kusitisha au kuzuia kwa muda, kwa sehemu au kwa jumla, dhidi ya sehemu yoyote ya Jukwaa la Bolt inayohusiana na akaunti yako:
10.1.1. endapo kutakuwepo na kutokutimiza wajibu wako katikaMasharti ya Jukwaa;
10.1.2. pale Bolt itakuwa inafanya uchunguzi kuhusu:
10.1.2.1. wajibu wa Bolt wa kisheria au wa kiusimamizi; au
10.1.2.2. ukiukaji unaoshukiwa wa Masharti haya ya Jukwaa.
ambapo katika hali hiyo, upatikanaji husika utasitishwa kwa muda wa uchunguzi pekee;
10.1.3. endapo umeshindwa kuhakiki utambulisho wako na/au taarifa za kuingia kwenye Jukwaa;
10.1.4. endapo Bolt itahitaji kufanya mabadiliko ili kufuata matakwa ya sheria au kanuni;
10.1.5. kupambana na changamoto za ghafla za kiufundi, mabadiliko, au maboresho; au
10.1.6. endapo Bolt inahitajika kuchukua taadhari za haraka kujilinda dhidi ya:
10.1.6.1. hatari ya ghafla kwa Watumiaji;
10.1.6.2. hatari za usalama mtandaoni (ikiwemo programu hasidi, barua taka, au ukiukaji wa usalama wa data);
10.1.6.3. kitendo kinachoshukiwa kuwa kinyume na sheria au haramu; au
10.1.6.4. madhara mengine makubwa kwenye uadilifu au sifa za Jukwaa la Bolt.
10.2. Bolt itajaribu kuwasiliana nawe kabla ya zuio hilo, labda kama kuna jambo la haraka, dharura, au sababu nyingine ya msingi, ikiwemo:
10.2.1. masuala ya afya na usalama;
10.2.2. uvunjifu uliokithiri au unaojirudia wa Masharti haya ya Jukwaa; au
10.2.3. endapo tutashindwa, au tumeshauriwa kutokufanya hivyo, kwa sababu za kiusimamizi au za kisheria.
10.3. Wakati umezuiliwa au umesimamishwa, utaweza (pale itakapopatikana) kufikia taarifa za kihistoria kuhusu Huduma za Usafiri Mtandaoni ambazo umepewa kupitia Jukwaa la Bolt.

**11. Namna uhusiano wetu unaweza kukoma**
11.1. Unaweza kusitisha uhusiano wako na Bolt katika Masharti haya ya Jukwaa mara moja na wakati wowote kwa kutoa taarifa husika kwa maandishi.
11.2. Bolt inaweza kukomesha uhusiano wake na wewe, moja kwa moja au kwa sehemu husika au aina ya kufikia, kama ifuatavyo:
11.2.1. kwa kukupatia notisi ya muda unaofaa;
11.2.2. mara moja, kwa kukupatia notisi husika, endapo:
11.2.2.1. kuna sheria mpya, kanuni, au wajibu umeanza kutumika (au mazingira kama hayo yaliyo nje ya uwezo wa Bolt) inayoilazimu Bolt kusitisha utoaji kwa sehemu au kwa jumla Jukwaa la Bolt mara moja;
11.2.2.2. Bolt inatimiza haki yake ya kwa mujibu wa sheria hsuika kukomesha uhusiano; au

11.2.2.3. kuna uvunjifu unaojirudia wa Masharti haya ya Jukwaa.
11.3. Baada ya kukomesha Masharti haya ya Jukwaa:
11.3.1. kwa ujumla, hautakuwa tena na haki ya kuingia kwenye Jukwaa la Bolt; au
11.3.2. kuhusiana na huduma fulani au kufikia sehemu fulani, husika (inapohitajika) hahautakuwa tena na haki ya kufikia sehemu za Jukwaa la Bolt zenye huduma hiyo.
11.4. Kukomeshwa kwa Masharti haya ya Jukwaa hakutaathiri haki yoyote iliyokuwepo au wajibu uliokuwepo kabla ya kukomesha.
11.5. Endapo Bolt itakomesha kuingia kwako kwenye Jukwaa la Bolt, unaweza kuwasilisha lalamiko au kuomba marejeo ya uamuzi kwa mujibu wa kanuni za ndani za kupokea malalamiko (tazama kipengele cha {14.8}).
11.6. Ili kuondoa mashaka yoyote, vipengele vinavyofuata vya Masharti ha ya Jukwaa vitaendelea kutumika kwa wakati wote ikiwemo baada ya kukomesha uhusiano wetu wote au kwa sehemu: {7} (malipo), {11} (uwajibikaji wako), {12} (wajibu wetu), {14} (haki miliki, notisi, migogoro, washirika wetu, kodi, tasfiri na mamlaka) na {15} (faharasa ya maneno yaliyofafanuliwa).

**12. Uwajibikaji wako**
12.1. Kwa kiwango kilichoruhusiwa kisheria, unakubali kufidia na kuirudishia Bolt madai, hasara, madeni, na gharama (ikiwa na pamoja na gharama za washauri wa kitaalamu wa Bolt na mawakala wa utekelezaji) zilizoingiwa kwa sababu ya matumizi yako ya Jukwaa la Bolt, ikiwemo na zinazohusu:
12.1.1. uvunjifu wowote wa wajibu wako kwa mujibu wa Masharti haya ya Jukwaa;
12.1.2. uharibifu wa mali au hasara ya pesa;
12.1.3. kusababisha hasara, biashara, mapato, mikataba, mawasiliano, heshima ya kibiashara, hadhi, au akiba iliyotarajiwa;
12.1.4. hasara yoyote inayotokana na kuingilia au matumizi ya Jukwaa la Bolt;
12.1.5. kupoteza, kuharibu au taarifa zisizo sahihi;
12.1.6. aina nyingine yoyote ya hasara isiyo ya moja kwa moja au hasara ya matokeo au uharibifu (kwa mfano, hasara ambazo isingekuwa rahisi kuzifikiria mwanzoni mwa uhusiano wetu);
12.1.7. tuhuma yoyote kwamba taarifa zozote zilizowasilishwa Bolt au zilizosambazwa kupitia Jukwaa la Bolt:
12.1.7.1. inavunja haki miliki ya mtu mwingine;
12.1.7.2. inavunja sheria yoyote au kanuni; na/au
12.1.8. matendo au kutokutenda kwa Abiria waliosafirishwa (au watakaosafirishwa) kupitia Huduma za Usafiri Mtandaoni ulizoomba.
12.2. Isipokuwa pale itakuwa imetajwa kivingine kwenye Masharti haya ya Jukwaa, unakubali kulipa kiasi chochote kinachopaswa kulipwa kwa Bolt mara tu utakapohitajika kwa mujibu wa Masharti haya ya Jukwaa (ikiwemo hasara yoyote iliyolipwa, malipo ya ziada, riba, au gharama za utekelezaji).
12.3. Malipo yako yoyote yatakayofanywa kwa kuchelewa kwa Bolt kwa mujibu wa Masharti haya ya Jukwaa yatalipwa pamoja na riba kwenye kiasi ambacho hakijalipwa, endapo imewekwa na Bolt, ambayo itakokotolewa kwa 2% (asilimia mbili) ya kiasi ambacho hakijalipwa kwa kila mwezi.

**13. Uwajibikaji wetu**
13.1. Bolt haitawajibika kwako kwa hasara yoyote, uharibifu, gharama, au malalamiko yatokanayo au yanayohusiana na:

13.1.1. matumizi yako ya Jukwaa la Bolt, au matumizi ya Jukwaa la Bolt na Dereva Aliyeteuliwa;
13.1.2. kutokupatikana, kuvurugika, au utendaji mbaya wa Jukwaa la Bolt;
13.1.3. matendo au mapungufu ya Mtumiaji yeyote wa Jukwaa la Bolt;
13.1.4. tovuti, maudhui, mifumo, au huduma (ikiwemo huduma za malipo) ambazo hazimilikiwi, kusimamiwa au kuendeshwa na Bolt, ikiambatana na ucheleweshwaji au makosa yanayosababishwa nazo;
13.1.5. taarifa zisizo sahihi au zilizopitwa na wakati ulizotoa Bolt;
13.1.6. maudhui ya tovuti za wengine, maudhui au programu;
13.1.7. kucheleweshwa kwa taratibu za malipo nje ya uwezo wa Bolt (mfano, ucheleweshwaji uliosababishwa na mtoa huduma za malipo mwingine); au
13.1.8. kuingia kwenye Jukwaa la Bolt kusikoruhusiwa kwa kutumia taarifa zako za kuingia kwenye Jukwaa.
13.2. Kuondolewa kwa wajibu katika kipengele cha {13.1} kunajumuisha, bila kikomo, kutohusika kwa chochote kwenye aina yoyote ya hasara au uharibifu, iwe ya moja kwa moja au kwa namna nyingine:
13.2.1. uharibifu wa mali au hasara ya fedha;
13.2.2. kutopata faida, hasara ya biashara, mikataba, mawasiliano, sifa ya biashara, hadhi, au akiba tarajiwa;
13.2.3. hasara yoyote itokanayo na muingiliano au matumizi ya Jukwaa la Bolt;
13.2.4. upotevu wa taarifa, uharibifu wa taarifa au taarifa zisizo sahihi; au
13.2.5. aina nyingine ya hasara au uharibifu wa moja kwa moja au wa namna nyingine (ikiwa ni pamoja na, kwa mfano, hasara ambayo isingeweza kufikiriwa wakati wa kuanza uhusiano wetu).
13.3. Wajibu wa juu kabisa wa Bolt kwako kwa jumla kwa mujibu wa Masharti haya ya Jukwaa hautazidi shilingi za kitanzania milioni moja (TZS. 1,000,000). Kiwango hiki kitatumika bila kujali idadi ya madai yaliyofanywa au idadi ya matukio yaliyosababisha wajibu huo.
13.4. Vikwazo vyote na misamaha ya uwajibikaji viliyowekwa kwenye Masharti haya ya Jukwaa vitatumika kwa kiwango cha juu kabisa kinachoruhusiwa kisheria.
13.5. Hakuna chochote katika Masharti haya ya Jukwaa kinachozuia au kuondoa wajibu wa Bolt kwenye:
13.5.1. kifo au majeraha kwa mtu vilivyosababishwa na uzembe wa Bolt; au
13.5.2. wajibu mwingine wowote ambao hauwezi kuzuilika au kusamehewa kisheria.

**14. Vipengele vingine muhimu**

Haki miliki

14.1. Haki miliki zote, alama za biashara, haki za kubuni, na haki nyingine miliki katika Jukwaa la Bolt - ikihusisha msimbo wa chanzo, hifadhidata, alama ya picha, miundo ya kuona (kwa pamoja, “Haki Miliki”) - zinamilikiwa na, au zimepewa leseni kwa Bolt. Kwa kutumia Jukwaa la Bolt, haupewi haki yoyote ya umiliki kwenye haki miliki. Haupaswi kutumia, au kuruhusu matumizi ya Haki Miliki bila kibali cha Bolt kwa maandishi

Notisi

14.2. Isipokuwa kama imeelezwa tofauti katika Masharti haya ya Jukwaa, notisi kwa Bolt kuhusiana na Masharti haya ya Jukwaa zitatolewa kwa njia ya maandishi kwenda Bolt kwa anuani iliyosajiliwa: Operesheni za Bolt, OÜ at Vana-Lõuna Tallinn 15, 10134, Estonia.

14.3. Bolt inaweza kutoa notisi kwako kuhusiana na Masharti haya ya Jukwaa kwa barua au barua pepe, kwa kutumia taarifa za mawasiliano za hivi karibuni ulizotoa kwetu kwa nyakati tofauti, au kupitia Programu ya Abiria.

14.4. Isipokuwa kama imeelezwa tofauti katika Masharti haya ya Jukwaa, notisi zitakazotolewa kuhusiana na Masharti haya ya Jukwaa lazima zitolewe kwa Kiswahili au Kiingereza na na itachukuliwa kuwa zimewasilishwa ipasavyo:

14.4.1. ikama imekabidhiwa kwa mkono, pale ambapo notisi itaachwa kwenye anuani inayohusika;

14.4.2. kama imetumwa kwa njia ya posta, siku inayofuata baada ya kuituma;

14.4.3. kama imetumwa kwa barua pepe, muda ambao barua pepe imetumwa; au

14.4.4. kama imetumwa kupitia Programu ya Abiria, muda ambapo notisi hiyo itakuwa kwako kupitia Programu ya Abiria.

14.5. Endapo muda ambao notisi inachukuliwa kuwasilishwa kwako ipasavyo kwa mujibu wa kipengele cha {14.4} itakuwa ni baada ya saa 11:00 jioni katika siku yoyote, au katika muda wowote kwa siku Jumamosi, Jumapili, au sikukuu, notisi hiyo itachukuliwa kuwa iliwasilishwa ipasavyo saa 03:00 asubuhi ya siku inayofuata ambayo siyo Jumamosi, Jumapili au sikukuu.

Utekelezaji

14.6. Bolt inaweza, kwa busara na kwa nia njema, kuamua kama kuna uvunjifu wa Masharti haya ya Jukwaa. Haki yoyote au hiari iliyotolewa au aliyonayo Bolt katika Masharti haya ya Jukwaa inaweza kutumiwa ipasavyo.

14.7. Bila kuzuia haki nyingine yoyote au uhiari uliotolewa kwa Bolt kwa mujibu wa Masharti haya ya Jukwaa, Bolt inaweza kwa busara na kwa nia njema, kuamua kama kitendo ni Kitendo cha Haramu cha Kidanganyifu Kilichokatazwa.

Migogoro

14.8. Endapo tumechukua hatua ambayo hukubaliani nayo kuhusiana na Masharti ya Jukwaa, unaweza kuwasiliana na timu yetu ya usaidizi kupitia Programu ya Abiria au kupitia sehemu ya notisi na migogoro iliyoko kwenye tovuti yetu.

14.9. Kwa kiwango cha juu kinachoruhusiwa kisheria, migogoro yoyote inayotokana na au inayohusiana na Masharti haya ya Jukwaa ambayo haitatuliwa kupitia mfumo wa ndani wa kutatua migogoro, itawasilishwa kwenye mahakama za Tanzania, ambazo zitakuwa na mamlaka pekee.

Uhamisho wa haki, ubadilishaji wa mkataba na uhamishaji wa majukumu

14.10. Hautahamamisha, kubadilisha au kutoa haki zako au majukumu yoyote katika Masharti ya Jukwaa bila ridhaa ya Bolt, ambayo ni lazima itolewe kwa maandishi kupitia Jukwaa la Bolt. Jaribio lolote la kufanya hivyo bila ridhaa halitakuwa halali.

14.11. Unakubali kuwa Bolt inaweza kugawa, kuhamisha au kurejea haki zetu chini ya Masharti haya ya Jukwaa muda wowote pasipo kupata ruhusa yako, na kuwa tunaweza kutoa utekelezaji wa wajibu wetu au kuteua washirika wetu kutumia haki zetu chini ya Masharti haya ya Jukwaa. Hii haitaathiri haki zako au wajibu wetu chini ya Masharti haya ya Jukwaa

Kodi ya Ongezeko la Thamani

14.12. Malipo yote, kiasi na kiwango kilichotolewa kwa mujibu wa Masharti haya ya Jukwaa, au kuonyeshwa kwenye Jukwaa la Bolt, zinajumuisha kodi ya ongezeko la thamani husika, isipokuwa kama imeelezwa tofauti.

Tafsiri

14.13. Vichwa vyote vya habari na maneno yaliyoelezewa katika Masharti haya ya Jukwaa ni kwa ajili ya marejeleo tu na haiathiri tafsiri ya kifungu chohote.

14.14. Katika Masharti haya ya Jukwaa, isipokuwa ilipoelezwa tofauti:

14.14.1. rejeleo la "kipengele" inamaanisha kipengele ndani ya Masharti haya ya Jukwaa;

14.14.2. rejeleo kwa "mhusika" inamaanisha mhusika katika Masharti haya ya Jukwaa, na "wahusika" itatafsiriwa ipasavyo;

14.14.3. maneno yaliyo katika umoja yanajumuisha wingi wake na kinyume chake;

14.14.4. rejeleo kwa jinsia moja inahusisha jinsia zote;
14.14.5. rejeleo kwa "mtu" inalenga binadamu, kampuni, ushirika, asasi, au taasisi nyingine ya kisheria;
14.14.6. marejeleo kwa "ikiwemo" au maelezo kama hayo hayazuii vitu vingine kujumuishwa.
14.15. Endapo kifungu chochote katika Masharti haya ya Jukwaa kitakutwa au kuamuliwa na mahakama au chombo kingine chenye mamlaka kuwa hakiwezi kutekelezeka, wahusika wanakubali kukibadilisha kifungu hicho na kifungu kilicho sahihi na chenye kutekelezeka, kadri itakavyowezekana, kulinda lengo la awali na lenye maana kibiashara.
14.16. Endapo kutakuwa na mgongano baina ya Masharti haya ya Jukwaa na makubaliano au mpango mwingine kati yako na Bolt, Masharti haya ya Jukwaa yatafuatwa labda kama imeelezwa tofauti.
14.17. Bolt inafanya kazi kama mtoaji wa Jukwaa mtandaoni kwa ajili ya huduma ya kuunganisha na machaguzi. Hivyo:
14.17.1. Hakuna chochote katika Masharti haya ya Jukwaa kinalenga kuonesha au kuamua kuwa Watoa Huduma au Madereva (Pamoja na Madereva Walioteuliwa) wanao wana wajibu kwa Bolt kufanya au kutoa Huduma za Usafiri Mtandaoni, au kwamba wanao uhusiano wa kiajira na Bolt.
14.17.2. Endapo kifungu chochote Masharti haya ya Jukwaa kitakutwa au kuamuriwa na mahakama au chombo kingine chenye mamlaka kuonesha wajibu binafsi wa kufanya au kutoa Huduma za Usafiri Mtandaoni au kuonesha uwepo wa mahusiano ya kiajira na Bolt, wahusika wanakubaliana kubadilisha kifungu hicho kwa kifungu kingine kilicho sahihi na kinachotekelezeka kitakachofuta mwelekeo huo, na kwa jinsi inavyowezekana, kutunza lengo la awali na lenye matokeo ya kibiashara.
Mamlaka
14.18. Kwa kiwango cha juu kinachoruhusiwa na sheria, Masharti haya ya Jukwaa na matumizi yako ya Jukwaa la Bolt vitaongozwa, na kutafsiriwa kwa mujibu wa sheria za Tanzania.

**15. Farahasa ya maneno**

Katika Masharti haya ya Jukwaa, maana zifuatazo zitatumika:
15.1. 'Bolt' ('sisi'/'yetu') inamaanisha Shughuli za Bolt OÜ iliyopo kwenye anuani iliyosajiliwa ya Vana-Lõuna Tallinn 15, 10134, Estonia.
15.2. 'Jukwaa la Bolt' inamaanisha teknolojia ya mfumo iliyotengenezwa na Bolt – ikiwemo Programu ya Abiria – ambalo kupitia humo Huduma za Usafiri Mtandaoni zinakutanishwa ndani ya Masharti haya ya Jukwaa, na kupitia vifaa vingine, taswira au huduma zinaweza kuwepo au kuunganishwa.
15.3. 'Ada ya Kughairisha/Ada ya Fidia' inamaanisha ada itakayotozwa kwa Wateja na Watoa Huduma pale ambapo Mteja ataahirisha ombi au kushindwa kwa namna nyingine kuingia kwenye makubaliano ya Huduma za Usafiri Mtandaoni baada ya Muda wa Kusubiri kuisha kama ilivyoelezwa katika kipengele cha {5.16}.
15.4. Makundi' inamaanisha makundi ya Huduma za Usafiri Mtandaoni yaliyopo kwenye Jukwaa la Bolt katika soko (inayoweza kuhusisha, kwa mfano, ikiwemo makundi ya 'magari ya umeme' au 'magari ya hadhi maalumu') na 'Kundi' inamaanisha aina yoyote katika hivyo.
15.5. 'Ada ya Usafi' inamaanisha ada inayotozwa kwa Wateja na Watoa Huduma pale ambapo Abiria amechafua gari wakati wa utoaji wa Huduma za Usafiri Mtandaoni kama ilivyoeelezwa zaidi katika kipengele cha {5.17}.
15.6. 'Kipindi cha Kukusanya' inamaanisha kipindi ambacho:
15.6.1. kinaanza pale Dereva anaonesha utayari wake wa kutoa au kutimiza Huduma za Usafiri Mtandaoni kwa Mteja husika kadri ya ombi la Mteja la Huduma za Usafiri Mtandaoni; na

15.6.2. kinakoma muda wa kuanza kwa Kipindi cha Safari au, kama ni mapema, pale ombi la Huduma za Usafiri Mtandaoni limeghairishwa au limesitishwa.
15.7. ‘Kipindi cha Kusubiria’ inamaanisha (kama inavyotumika) kipindi kilichowekwa katika Jukwaa la Bolt kuanzia pale Dereva anapoonesha utayari wake wa kutoa Huduma za Usafiri Mtandaoni kwa Mteja husika (yaani pale ambapo Mteja amelinganishwa na Dereva).
15.8. ‘Mteja’ inamaanisha mhusika anayeomba (na anaweza kupewa) Huduma za Usafiri Mtandaoni.
15.9. ‘Huduma za Usafirishaji’ inamaanisha huduma za usafirishaji zinazotolewa na Watoa Huduma kwa Wateja kwa ajili ya kusafirisha bidhaa kutoka eneo la kupokelea kwenda eneo la mwisho/kikomo bila kusafirisha Msafiri, kama ilivyoelezwa kutoka kipengele cha {5.25} mpaka {5.29}.
15.10. ‘Tabia ya Kibaguzi’ inamaanisha tendo lolote – ikiwemo kauli, matendo, na vitendo kwa wengine – ambacho kinaonesha upendeleo, iathari, au chuki na sifa zinazolindwa kama rangi, ukabila, uraia, jinsia, mwelekeo wa kijinsia, utambulisho wa kijinsia, dini, ulemavu au umri.
15.11. ‘Dereva’ inaamisha mtu aliyesajiliwa na Bolt na wewe kufikia na kupitia fursa za kutoa Huduma za Usafiri Mtandaoni kwa niaba ya Mtoa Huduma
15.12. ‘Nauli’ inamaanisha gharama inayolipwa kwa ajili ya Huduma za Usafiri Mtandaoni.
15.13. ‘Kipindi cha Safari’ inamaanisha kipindi kitumikacho:
15.13.1. kinaanza pale Dereva anapofika eneo la la kuchukulia na kuanza Huduma za Usafiri Mtandaoni kwa kumchukua Mteja (au Abiria pale inapohusika) na kukubali kumsafirisha hadi eneo la mwisho/kikomo lililoombwa; na
15.13.2. kinakoma pale Huduma za Usafiri Mtandaoni zinaisha au kufikia mwisho kwa sababu nyingine yoyote.
15.14. ‘Abiria’ inamaanisha mtu yeyote ambaye anasafirishwa au atakaye safirishwa kama abiria kwa mujibu wa kifungu cha Huduma za Usafiri Mtandaoni.
15.15. ‘Malipo’ inamaanisha kwa pamoja:
15.15.1. Nauli, Tozo za Barabarani, Ada za Kughairisha, na Ada za Usafi (kwa ujumla au kwa sehemu) ambazo unatakiwa kulipa kwa Watoa Huduma, pamoja na bakshishi, kwa ajili ya Huduma za Usafiri Mtandaoni ulizokubali kufanya; na
15.15.2. Ada za Jukwaa amabazo unatakiwa kulipa Bolt pamoja na bakshishi zinaohusiana na Huduma za Usafiri Mtandaoni ulizokubali kufanya.
15.16. ‘Njia ya Malipo’ inamaanisha njia ya kufanya Malipo kupitia Jukwaa la Bolt ambayo ni lazima iwe kadi ya mkopo au kadi ya malipo ya moja kwa moja (au njia nyingine ya malipo inayokubalika katika Programu ya Mteja) iliyo kwenye jina lako au ulyoidhinisha, au inayohusiana na taarifa za malipo mfano anuani yako
15.17. ‘Ada ya Jukwaa’ inamaanisha ada unatakayotozwa na Bolt kwa wewe kutumua Jukwaa la Bolt kama ilivyoelezwa zaidi katika kipengele cha {6}
15.18. ‘Masharti ya Jukwaa’ inamaanisha ujumla wa vigezo na masharti haya yanayojulikana kama ‘Masharti ya Jukwaa la Huduma za Usafiri Mtandaoni: Wateja (TZ) (kwa Kiswahili) (kuanzia 31.02.2026)’.
15.19. ‘Matendo ya Udanganyifu Yaliyokatazwa’ inamaanisha matumizi yoyote ya Jukwaa la Bolt yanayoonesha nia – au jaribio lolote – la kudanganya, kuharibu, kuumiza mtu yeyote au Jukwaa la Boltl, au kuharibu au kutoa sifa yoyote ya nyongeza kinyume cha utaratibu kwenye Jukwaa la Bolt. Hii inahusisha:
15.19.1. ombi, kubalio au kumaliza Huduma za Usafiri Mtandaoni katika namna ambayo inaonesha kuwa iliyopitiliza, ya kutengeneza au iliyopangwa visivyo; na
15.19.2. tabia inayojirudia inayoonesha kuwa imetengenezwa kudanganya uhalisia wa uhitaji au nia ya kutoa Huduma za Usafiri Mtandaoni.

15.20. ‘Vipindi vya Kuomba Huduma’ inamaanisha kwa pamoja (kuhusiana na ombi la Huduma za Usafiri Mtandaoni) Kipindi cha Kukusanya na Kipindi cha Safari.
15.21. ‘Mtoa Huduma’ inamaanisha mtu au taasisi ambayo imejisajili kwa Bolt ili kufikia na kupitia fursa za kutoa Huduma za Usafiri Mtandaoni ndani ya Tanzania kwa faida yao wenyewe.
15.22. ‘Huduma za Usafiri Mtandaoni’ inamaanisha huduma za usafirishaji zinazotolewa na Watoa Huduma kwa Wateja ambazo zinapangwa kupitia Jukwaa la Bolt (ikiwemo Huduma za Usafirishaji).
15.23. ‘Malipo ya Tozo’ inamaanisha malipo yanayopaswa kulipwa kwa Watoa Huduma kama tozo ya ziada kwa sababu ya njia ya Huduma za Usafiri Mtandaoni inayosababisha gharama ya ziada au usumbufu kwa mfano safari kupitia barabara na madaraja ya kulipia au safari zinazohitaji ada ya kuegesha gari kwenye kiwanja cha ndege.
15.24. ‘Watumiaji’ inamaanisha watumiaji wote na wanufaika wa Jukwaa la Bolt ikiwemo Watoa Huduma, Madereva, Wateja na Abiria.
15.25. ‘Wewe’ (au ‘wewe’) inamaanisha Mteja ambaye anahusika na Masharti yay a Jukwaa.

Mwisho wa Masharti ya Jukwaa